TANGAZO LA SERIKALI NA. 716 la tarehe 02/12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA IPOLE YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Ipole ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka I1 iliyopo katika bonde la Mpunga kupita barabara ya Mbeya kwenye majira-nukta 470592E, 9357661N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi-Kaskazini sambamba na bonde katika uelekeo wa W80$^{0}$5’20”N kwa umbali wa kilomita 1.3 hadi alama ya mpaka I2 iliyopo barabara ya Mpanda katika majira-nukta 469268E, 9358567N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa N105$^{0}$7’0”W kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi alama ya mpaka I3 iliyopo barabara ya zamani ya Mpanda katika majira-nukta 469220E 9359010N; baada ya hapo mpaka unanyooka kwa umbali wa kilomita 2.9 hadi katika alama ya mpaka I4 iliyopo barabara ya Mihamakumi katika majira-nukta 468676E, 9361894N; baada ya hapo mpaka

*Tagazo la seriakli na. 716 (linaendelea)*

unanyooka kwa umbali wa kilomita 1.06 hadi katika alama ya mpaka I5 iliyopo barabara ya Makazi na Kaskazini-Magharibi mwa eneo la Makazi yenye majira-nukta 468400E, 9362947N; baada ya hapo mpaka utaelekea Mashariki-Kaskazini katika uelekeo wa E95$^{0}$6’20” kwa umbali wa kilomita 3.1 hadi katika alama ya mpaka I6 iliyopo barabara ya Tabora-Mpanda katika majira-nukta 471529E, 9364387N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa S90$^{0}$6’0” kwa umbali wa kilomita 3.5 hadi alama ya mpaka I7 iliyopo barabara ya Kabanga katika majira-nukta 473152E, 9360918N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa S95$^{0}$6’20” kwa umbali wa kilomita 1.6 hadi katika alama ya mpaka I8 iliyopo barabara ya zamani ya Kabanga yenye majira-nuta 471697E, 9359341N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 1.7 hadi ulipoanzia”.

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*